FUNZO LA 37

1. Je, ni nani aliyeandika vitabu tano vya kwanza vya Biblia?
-Musa.

2. Je, Musa alijuaje alichopaswa kuandika?
-Mungu alimuelekeza Musa kuandika kile ambacho Mungu alitaka kiandikwe.

3. Je, Waisraeli walipokuwa wakisafiri katika jangwa, walijuaje njia waliostahili kufuata?
-Mungu aliwaongoza.

4. Je, Mungu alikuwa akiwaelekeza wapi Waisraeli?
-Mungu alikuwa akiongoza Waisraeli kuelekea Kanaani, nchi aliyoahidi baba yao Ibrahamu.

5. Waisraeli walipofika katika mpaka wa Kanaani, Mungu alimwambia Musa afanye nini?
-Mungu alimwambia Musa achangue mtu mmoja kutoka kila kabila ya Israeli ili wakaipeleleze ile nchi.

6. Je, kwa nini wale kumi ambao hawakumwamini Mungu hawakutaka kwenda Kanaani?
-Wale kumi waliogopa watu wakubwa na wenye nguvu waliokuwa wakiishi Kanaani.
-Wale kumi hawakuamini kuwa Mungu alikuwa na uwezo wa kuwashinda watu walioishi Kanaani.
-Wale kumi hawakuamini ahadi ya Mungu ya kuwapa Israeli nchi ya Kanaani.



7. Je, kwa nini Yoshua na Kalebu walitaka kuingia nchi ya Kanaani?
-Kalebu na Yoshua hawakuogopa watu wakubwa na wenye nguvu waliokuwa katika nchi ya Kanaani.
-Kalebu na Yoshua waliamini kuwa Mungu ni mwenye nguvu zaidi na angewashinda watu waliokuwa wakiishi Kanaani.
-Kalebu na Yoshua waliamini ahadi ya Mungu ya kuwapa Waisraeli nchi ya Kanaani.

8. Je, iwapo hatutaamini ujumbe wa Mungu, tunamwitaje Mungu?
-Muongo.

9. Je, kwa sababu Waisraeli walikataa kumwamini Mungu, ni nani pekee aliyekubaliwa kuingia Kanaani?
-Ni Kalebu, Yoshua na watoto wa Waisraeli.

10. Je, kwa sababu Waisraeli walikataa kumtii Mungu, Mungu aliwaadhibu vipi Waisraeli?
-Hawakuingia Kanaani.
-Wote walikufa jangwani.

-Kwa sababu Waisraeli walikataa kumwamini Mungu, hawakuingia Kanaani bali walizunguka jangwani.

-Waisraeli walipofika Kadeshi, hapakuwa na maji.

-Je, unafikiri Waisraeli walifanya nini?

Tusome Hesabu 20:1-5

1-Kisha wana wa Israeli, mkutano wote, wakaingia bara ya Sini, katika mwezi wa kwanza, watu wakakaa Kadeshi; Miriamu akafa huko, akazikwa huko.

2-Na hapo hapakuwa na maji kwa ule mkutano; wakajikusanya juu ya Musa na juu ya Haruni.

3-Watu wakashindana na Musa, wakanena, wakisema, Ingalikuwa heri kama tungalikufa wakati ule ndugu zetu walipokufa mbele za Bwana!

4-Mbona mmewaleta kusanyiko la Bwana hata jangwa hili ili tufe huku, sisi na wanyama wetu?

5-Na mbona mmetupandisha kutoka Misri ili kutuleta hata mahali hapa pabaya? Si mahali pa mbegu, wala tini, wala mizabibu, wala makomamanga; wala hapana maji ya kunywa.

-Je, Waisraeli walipokosa maji, walimwamini Mungu awape maji?
-La.

-Je, Waisraeli walifanya nini?
-Waliwalaumu Musa na Haruni.

-Je, Waisraeli walipaswa kufanya nini iwapo hakukuwa na maji?

-Walipaswa kumuomba Mungu awape maji.

-Hapo awali Mungu aliwapa maji kutoka kwa mwamba.

-Je, kwa nini Waisraeli hawakumuomba Mungu awape maji?



-Kwa sababu hawakumwamini Mungu.
-Hata sasa, watu wengi ni kama Waisraeli.

-Hata kama Mungu analeta mvua na kufanya mahindi yakue, bado hawamwamini Mungu.

-Je, Musa na Haruni walifanya nini wakati hakukuwa na maji?

Tusome Hesabu 20:6

6-Musa na Haruni wakatoka pale palipokuwa mkutano, wakaenda hata mlangoni pa hema ya kukutania, wakaanguka kifudifudi; utukufu wa Bwana ukawatokea.

-Musa na Haruni walimwamini Mungu.
-Musa na Haruni walimuomba Mungu awape maji.

-Je, Musa na Haruni waliweza kuwapa Waisraeli maji?
-La.

-Je, kwa nini Musa na Hruni hawakuwa na uwezo wa kuwapa Waisraeli maji?

-Kwa sababu walikuwa jangwani.

-Je, iwapo Mungu angewapa Waisraeli maji, nini kingefanyika?
-Waisraeli wote wangekufa.

-Je, Mungu aliwapa Waisraeli maji?

Tusome Hesabu 20:7-8

7-Bwana akasema na Musa, akinena,

8-Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako, ukauambie mwamba mbele ya macho yao utoe maji yake, nawe utawatokezea maji katika mwamba, na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao.

-Kwa sababu Mungu aliwapenda Waisraeli, aliwapa maji.

-Je, Mungu alimuamuru Musa afanye nini ili apate maji?
-Mungu alimuamuru Musa anene na mwamba.

-Hapo awali, Waisraeli walipoitaji maji, Mungu alimuamuru Musa kuugonga mwamba.

-Sasa, Mungu alimuamuru Musa kunena na mwamba.

-Je, Musa alifanya nini?

Tusome Hesabu 20:9-11

9-Musa akaitwaa hiyo fimbo kutoka mbele za Bwana kama alivyomwamuru.

10-Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia, Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?

11-Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili; maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia.



-Je, Musa alinena na mwamba?
-La.

-Je, Musa alifanya nini?
-Aliugonga huo mwamba mara mbili.

-Je, kwa nini Musa aliugonga mwamba?
-Kwa sababu alikasirishwa na Waisraeli.

-Je, Musa alikosa kumtii Mungu?
-Ndiyo.

-Je, Mungu aliwaambia nini Musa na Haruni?

Tusome Hesabu 20:12

12-Bwana akamwambia Musa na Haruni, Kwa sababu hamkuniamini mimi, ili kunistahi mbele ya macho ya wana wa Israeli, basi kwa sababu hiyo, hamtawaingiza kusanyiko hili katika ile nchi niliyowapa.

-Kwa sababu Musa na Haruni hawakunena na mwamba ila wakaugonga, Mungu aliwaadhibu?
-Ndiyo.

-Je, Mungu aliwaadhibu vipi Musa na Haruni?
-Mungu aliwaambia kuwa hawataingia katika nchi ya Kanaani.

-Wakati wa Haruni wa kufa ulipofika, Mungu alimwambia Musa ampeleke Haruni juu ya mlima uliokuwa karibu.

Tusome Hesabu 20:23-25 & 28

23-Bwana akanena na Musa na Haruni katika mlima wa Hori, karibu na mpaka wa nchi ya Edomu, akawaambia,

24-Haruni atakusanywa awe pamoja na watu wake; kwa sababu hataingia katika nchi niliyowapa wana wa Israeli, kwa sababu mliasi kinyume cha neno langu hapo penye maji ya Meriba.

25-Uwatwae Haruni na mwanawe Eleazari uwalete juu ya mlima wa Hori;

28-Kisha Musa akamvua Haruni mavazi yake, akamvika mwanawe Eleazari mavazi hayo; Haruni akafa huko katika kilele cha mlima; Musa na Eleazari wakatelemka mlimani.

-Juu ya mlima, Haruni akafa.

-Je, Haruni aliingia nchi ya Kanaani?
-La.

-Kwa nini hakuingia?
-Kwa sababu hakumtii Mungu.

-Je, Mungu alitimiza Neno lake?
-Ndiyo.
-Mungu kamwe hutimiza Neno lake.

-Je, ni nani aliyechukua nafasi ya Haruni kama kuhani mkuu?
-Mwana wa Haruni, Elieza.

-Baadaye kidogo, Waisraeli tena walilalamika.



Tusome Hesabu 21:4-5

4-Wakasafiri kutoka mlima wa Hori kwa njia ya Bahari ya Shamu; ili kuizunguka nchi ya Edomu, watu wakafa moyo kwa sababu ya ile njia.

5-Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu.

-Ingawaje Mungu aliwapa Waisraeli maji, walizidi kulalamika.

-Je, kwa sababu Waisraeli walizidi kulalamika, Mungu aliwafanyia nini?

Tusome Hesabu 21:6

6-Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa.

-Mungu aliwaadhibu Waisraeli kwa kutuma nyoka wengi na wenye sumu miongoni mwao.

-Hao nyoka wenye sumu walikuwa kila mahali.

-Wengi wa hao Waisraeli waliumwa na hao nyoka na wakafa.
-Je, dhambi inafananaje na hao nyoka?

-Kama vile nyoka walivyowauma watu na wakafa, ndivyo dhambi huuma watu na wanakufa.

-Je, Waisraeli waliweza kuhepa nyoka wenye sumu?
-La.

-Kwa nini hawakuweza?

-Kwa sababu nyoka wenye sumu walikuwa kila pahali.

-Mungu anapoamua kuwaadhibu wenye dhambi, hakuna wanapoweza kutorokea.

-Je, katika siku za Nuhu, kulikuwa na pa kujificha kwa wale waliokuwa nje ya mashua?
-La.

-Je, katika siku za Sodoma na Gomora, kulikuwa na pa kujificha kwa wale waliokuwa ndani ya hiyo miji?
-La.

-Je, kulikuwa na pahali pa kujificha kwa mke wa Lutu aliyeangalia nyuma kwa miji ya Sodoma na Gomora?
-La.

-Wakati Mungu anapoamua kuwaadhibu watu wasiomwamini, hakuna pahali wanapoweza kutorokea.

-Wakati Waisraeli wengi walipokufa, wengine walifanya nini?

Tusome Hesabu 21:7

7-Watu wakamwendea Musa, wakasema, Tumefanya



dhambi kwa sababu tumemnung'unikia Mungu, na wewe; utuombee kwa Bwana, atuondolee nyoka hawa. Basi Musa akawaombea watu.

-Je, Waisraeli walikiri dhambi yao?
-Ndiyo.

-Je, Waisraeli walimwomba Musa na Mungu awasaidie?
-Ndiyo.

-Je, Waisraeli waliweza kujiokoa kutoka kwa wale nyoka?
-La.

-Je, Musa aliweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa wale nyoka?
-La.

-Je, ni nani pekee aliyeweza kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa wale nyoka?
-Mungu.

-Je, Mungu aliwasaidi Waisraeli?

Tusome Hesabu 21:8-9a

8-Bwana akamwambia Musa, Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi.
9-Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti,

-Je, Mungu alimwambia Musa afanye nini ili awaokoe Waisraeli?

-Atengeneze nyoka wa shaba na amuangike juu ya mti.

-Je, iwapo Waisraeli lazima waokolewe, wangefanya nini?

-Wamwangalie nyoka wa shaba aliyeinuliwa mtini.

Tusome Hesabu 21:9b

9-Hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi.

-Je, Waisraeli waliomwangalia yule nyoka wa shaba mtini, waliishi?

-Ndiyo.

-Je, kama Waisraeli wangeomba na wasimtazame yule nyoka wa shaba, wangeishi?
-La.

-Je, iwapo Waisraeli wangemtolea Mungu kafara ila wasimtazame yule nyoka wa shaba, wangeishi?
-La.

-Ili waokolewe, Waisraeli waliitajika kutii kile ambacho Mungu aliwaambia.



-Ili waokolewe, Waisraeli waliitajika kufuata njia ya Mungu.

-Ili waokolewe, Waisraeli waliitajika kumtazama nyoka wa shaba mtini.

-Je, yule nyoka wa shaba alikuwa na uwezo wa kuwaokoa Waisraeli?
-La.

-Je, ni nani pekee aliyekuwa na uwezo wa kuwaokoa Waisraeli?
-Mungu.

-Mungu aliwaokoa Waisraeli wote waliomtazama nyoka wa shaba mtini.

-Je, dhambi ya Waisraeli ilistahili kifo?
-Ndiyo.

-Je, ingawaje dhambi ya Waisraeli ilistahili kifo, Mungu aliwafanyia nini Waisraeli waliomtazama nyoka?

-Mungu aliwaokoa.